JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA

IMEIDHINISHWA KWA KIWANGO CHA ISO 9001:2015

TAARIFA KWA UMMA

UWASILISHAJI WA MAOMBI YA UHUISHWAJI WA LESENI, VYETI, IDHINI NA RUHUSA KWA WAKATI

Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imebaini kuwa baadhi ya watoa huduma, wataalamu wa usafiri wa anga na watumiaji wengine wa huduma za usafiri wa anga wanaosimamiwa na Mamlaka huwasilisha maombi ya uhuishaji wa leseni, vyeti, idhini, muda mfupi kabla ya kuisha kwa muda wa matumizi wa nyaraka hizo. Hali hii inapunguza muda unaohitajika kwa Mamlaka kufanya tathmini, ukaguzi na huduma nyingine zinazohitajika kabla ya kuhuishwa.

Hivyo, Mamlaka inawakumbusha watumiaji wa huduma za usafiri wa anga wote wanaohusika kuwasilisha maombi ya uhuishaji ndani ya muda uliowekwa na Kanuni husika za Usafiri wa Anga.

Ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa wakati, watoa huduma, wataalamu wa usafiri wa anga na watumiaji wengine wote wa huduma za usafiri wa anga wanahimizwa kufuatilia muda wa uhalali wa nyaraka zao na kuwasilisha maombi kamili ya uhuishaji kupitia Mfumo wa Huduma za Usafiri wa Anga (CASP) ndani ya muda.

Aidha, waombaji wanakumbushwa kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazowasilishwa katika maombi yao ni sahihi na kamili. Hii itapunguza urejeshwaji wa maombi kwa ajili ya marekebisho au ukamilishaji na hivyo kuepusha ucheleweshaji usio wa lazima katika kushughulikia maombi.

Watumiaji wa huduma za usafiri wa anga husika wanakumbushwa pia kuwa kuwasilisha maombi kwa kuchelewa hakutailazimisha Mamlaka kuharakisha au kupunguza taratibu za tathmini na utoaji wa idhini zilizowekwa. Ni wajibu wa kila mwombaji kuhakikisha mwendelezo na uhalali wa leseni, vyeti, idhini na ruhusa zake.

Imetolewa tarehe 03 Oktoba 2026.

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Sat Oct 03 16:59:12 EAT 2026

Dkt.Jabiri K. Bakari
Mkurugenzi Mkuu

Aviation House, Mwisho wa Barabara Nyerere/Kitunda, S.L.P 2819, Dar es Salaam, Tanzania
Email: dg@tcaa.go.tz Telephone: +255-282 560333